


**TRUTH
CENTERED
TRANSFORMATION**

MODULE 2



Ufalme wa Mungu Mwongozo wa mwalimu

Truth Centered Transformation-Module2: Kingdom of God version 3 Copyright©2012 Reconciled World, Phoenix, Arizona, United States of America.www.reconciledworld.org

Kazi hii inapatikana chini ya Creative Commons Attribution-ShareAlike3.0 license.Unaweza kuitumia kurekebisha na kusambaza kazi hii chini ya kanuni zifuatazo:

Kunukuu—Lazima unukuu kwa kusema yafuatayo: Copyright©2012. Published by the Reconciled World (www.reconciledworld.org) undertermsoftheCreative CommonsAttribution-ShareAlike3.0license.Kwa habari zaidi fuata www.creativecommons.org.

Kazi hii haiuziki.



Ukitaka kutafsiri wasiliana na info@tctprogram.org.

Mistari yote ya Biblia inatokana na NIV the Holy Bible, New International Version®, NIV®. Copyright©1973,1978,1984,2011 by Biblica, Inc. TM Used by permission of Zondervan. All rights reserved worldwide. www.zondervan.com The “NIV” and “New International Version” are trademarks registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. TM

Shukrani

Mawazo kwenye mafunzo hayo si ya kwangu. Ninaendeleza kazi za walionitangulia. Vipindi vimetokana na kazi ya DiscipleNations Alliance (disciplenations.org). Makenisa mengi yaliyosoma walisaidia kubadilisha vipindi kutokana na maoni yao au kutokuelewa kwao. Ninawashukuru kwa subira yao wakati nilipojifunza kuwasiliana juu ya ukweli.

Mambo mengi yaliyomo humu yanatokana na kitabu cha Bob Moffitt "If Yesu was Mayor." Mawazo na picha za somo la 2, 5 na 6 hutokana na kitabu hiki. Somo la 3, maadili ya ufalme linatokana na mwongozo wa kusoma biblia "God's Unshakable Kingdom" (Kingdom Lifestyle Bible Studies) by Darrow Miller, Bob Moffitt and Scott Allen.

Wakati wengine wamenipa mawazo makosa ni yangu mimi mwenyewe. Naomba unijulishe ikiwa mabadiliko yatakiwa kuboresha masomo.

Yaliyomo

Somo la 1: Ufalme wa Mungu.....	3
ufalme wa Mungu ni nini	3
kutii kwa mambo yote.....	4
kujenga ufalme wa Mungu.....	5
Somo la2: Jamii za ufalme	6
ufalme duniani	6
Mungu ni mtawala wa jamii zetu.....	6
Yesu kama kiongozi wa jamii.....	8
mabadiliko ndani ya jamii kwenye maeneo yote manne.....	8
Somo la 3:Maadili ya ufalme.....	10
Kanuni za msingi.....	10
kutekeleza biblia kwenye kila eneo la maisha yetu.....	12
Kutafuta kanuni za Mungu	14
Somo la4: Maadili ya ufalme na kazi.....	15
mtazamo wa biblia kuhusu kazi.....	16
aina za kazi.....	16
Mungu anajali tunavyofanya kazi.....	18
Somo la5: Kujenga ufalme wa Mungu.....	20
Inaanzia kwetu.....	20
jamii iliyobadilika.....	20
Tutabadilishaje jamii yetu.....?	21
BrudaLawrence.....	22
kutoka watu hadi familia hadi jamii.....	23
Familia.....	24
Jamii.....	24
mifano mingine ya waliojenga ufalme wa Mungu.....	26
namna ya kuwa mjenzi wa ufalme.....	28
Somo la6: Kazi ya kanisa kwenye ujenzi wa ufalme wa Mungu.....	30
kuwawezesha watu.....	31
kwa nini wote tuhudumie?.....	32
kubadilisha familia.....	33
kubadilisha jamii.....	33
Somo la7: Programu ya mabadiliko kwa msingi wa ukweli.....	36
maono ya mradi.....	36
kuwezesha makanisa.....	37
kubadilisha jamii.....	38
maeneo ya mabadiliko	39
mbinu,,.....	40
maada ijayo ya mafunzo.....	40
Somo la8: Hatua zifuatazo.....	41
umuhimu wa mipango.....	41
Mikutano.....	42
Vitendo vya upendo.....	42
Hatua za kupanga vitendo vya upendo.....	43

Kabla ya kuanza

Maandalizi ya kufundisha somo

1. Usome **mwongozo wa mwalimu** mara kadhaa kwa umakini. Uandike mambo muhimu pembeni.
2. Angalia **malengo** ujue wanafunzi wanapaswa wajifunze nini
3. Soma **mistari yote** kabla ya muda.
4. Angalia **vifaa vipi** huhitajika kwenye kila kipindi na utengeneze nakala ya vifaa kwa wanafunzina uandaa vioneshi vinavyopaswa kutumika.
5. Uhakikishe unajua kila **kitendo** kwenye somo (maigizo, michezo, vioneshi). Unaweza kufanya mazoezi na marafiki na familia.
6. Uchukue muda **kumwomba Mungu** awaandae wanafunzi, wanafunzi wasikie ujumbe wa Mungu na akusaidie kufundisha, Kumbuka kwamba watu hubadilishwa kwa uwezo wa Mungu peke yake.

Ufundishaji bora

1. Ufike mapema uandae vifaa vyako na eneo lako
2. Usiharakishe kupitia mada. Uwe na muda kwa ajili ya majadiliano, vitendo na mapumziko. Lengo ni kuwa na muda kwa watu kuelewa na kushiriki mafunzo. Uende mada hadi mada ukihakikisha kwamba kila mtu anaelewa. Masomo mengine yanaweza kuhitaji nusu siku au siku nzima ya ziada.
3. Urudie mara nyingi. Mwanzoni mwa kila kipindi uwafanye wanafunzi warudie kila kitu walichokisoma tangu masomo yaanze. Marudio huwasaidia watu kukumbuka walichokisoma.
4. Fuata mwongozo wa mwalimu na maandalizi yako.
5. Uhakikishe kuwakilisha sehemu zote nne za kipindi.
 - a. Tambulisha maada–vitendo vitaunganisha maada na mambo yaliyotangulia.
 - b. Toa habari mpya–kuna njia kadhaa kushirikisha habari mpya.
 - c. Uwape wanafunzi kitu cha kujifunzia– vitendo vyawasaidia kuelewa vizuri zaidi wakifanya kazi na wengine, kwa kutengeneza kitu au kutumia habari mpya kwa namna mmoja au nyingine.
 - d. Uunganishe habari na maisha yao–hii ni hatua ya utekelezaji inayomsaidia mwanafunzi kuamua njia ya kutumia walichojifunza maishani mwao. Kujifunza bila utekelezaji hakuletei mabadiliko na hakusaidii chochote.
6. Upitie tena kanuni za elimu ya watu wazima na mengineyo ulichofundishwa kwenye mafunzo ya maendeleo ya wawezeshaji
 - a. Utoe maelezo yanayoeleweka
 - b. Uulize maswali mengi
 - c. Uwashukuru watu kwa kushiriki
 - d. Usiwaambie kitu ambacho waweza kujifunza kwa kugundua wenyewe

- e. Uendeleze wanachojua na uheshimu uzoefu wao
- f. Uwe na subira na uwape muda wa kujibu
- 7. Umtie moyo kila mmoja kushiriki na kutoa maoni na uzoefu kwenye majadiliano. Uwatie moyo wenye aibu bila kuwaogopesha zaidi.
- 8. Umwombe Mungu siku nzima awaoneshe mambo mapya wewe pamoja na wanafunzi wako.

Matumizi ya mwongozo wa mwalimu

1. **Malengo na vifaa:** kila kipindi kinaanzia hapo.
 - a. **Malengo**—wanafunzi wanapaswa kuyaweza mwishowni wa kila kipindi. Ni vizuri ukijiuliza kama malengo yamefikwa mwisho wa kipindi. Urudie mambo muhimu mara kwa mara ili kuwasaidia kukumbuka.
 - b. **Vifaa**—vifaa vinaorodheshwa kwa kila kipindi pamoja na vioneshi na vitu vya kuwapa wanafunzi. Unaweza kuchagua kumpa kila mwanafunzi mwongozo kamili wa mwanafunzi au unatoa nakala chache kutokana na maelekezo yanayotolewa. Pia uwe na karatasi kubwa au ubao ukiwa na wanafunzi wengi.
2. **Maelekezo kwa mwalimu:** Kuna maelekezo kukusaidia kuongoza kipindi vizuri. Hayo si kwa ajili ya wanafunzi. Uyasome ili uweze kuongoza majadiliano na vitendo. Baadhi ya maswali yana majibu kukusaidia kuwaongoza wanafunzi kupata majibu sahihi. Hayo si majibu mazuri pekee ni baadhi tu.
3. **Kumudu wakati na mtiririko:** muda haujawekwa kwa kila kipindi.
 - a. Utumie muda wa kutosha ili watu waelewe kinachofundishwa. Ni muhimu zaidi kuhakikisha watu wameelewe kuliko kufuata muda.
 - b. Kumbuka kuwa na muda wa kufungua kwa maombi ushuhuda kujadili matatizo na maombi ya pamoja.

Somo la 1 : Ufalme wa Mungu

Malengo makuu

1. Kuelewa kwamba ufalme wa Mungu unakuwepo pale tunapotii amri za Mungu kwa ukamilifu
2. Kuelewa kwamba ufalme unakua ikiwa watu wengi zaidi wanamtii Mungu nasi tunamtii kwa ukamilifu zaidi

Vifaa

1. hakuna

Ufalme wa Mungu ni nini?

Yesu alipokuwa duniani ametushirikisha mpango wake. Mpango huo unatajwa mara 98 kwenye agano jipya. Yesu alisema mpango huo ndiyo sababu alitumwa na anawatuma wafuasi wake waufundishe pia. Paulo amezungumzia na tunatiwa moyo kuuomba.

- Unajua ni nini?

JADILI KWENYE VIKUNDI VIDOGO

Soma mistari ifuatayo ujibu maswali:

- Mathayo 10:5-8 — Yesu aliwatuma wafuasi wake wafundishe nini?
- Luka 4:43 — Kwa nini Yesu alitumwa?
- Matendo ya mitume 1:3 — Kwenye siku arobaini zake za mwisho duniani Yesu alifundisha kuhusu nini?
- Matendo ya mitume 28:30-31 — Paulo amefundisha nini?

Mpango wa Mungu ni kujenga ufalme wa Mungu. Kama tunavyoona kwenye mistari hii Yesu na Paulo walifundisha hayo. Yawe muhimu kwetu pia. Hata hivyo wengi wetu hatuelewi maana ya ufalme wa Mungu.

- Umgeukie mwenzio ujiulize jinsi utakavyoeleza ufalme wa Mungu kwa Mkristo mpya

Ushirikishe kikundi kizima majibu.

Ufalme wa Mungu si ngumu kueleza. Ufalme wa Mungu ni pale ambapo Yesu ni mfalme na sheria zake hufuatwa. Kwa hiyo kokote tunakoona watu wakimtii Mungu na kufuata matakwa yake kuna sehemu ya ufalme wa Mungu. Ufalme wa Mungu hautakamilika hadi Yesu atakaporudi na kila kitu kitatengenezwa upya bila dhambi.

kutusaidia kuelewa tukumbuke Thailand. Thailand ni ufalme: wana mfalme na mfalme akiongea watu wa Thailand wanasikiliza Alisema anapenda rangi ya njano na sasa watu huvaa mashati ya njano kila Jumatatu. Alisema mke wake anapenda zambarau sasa watu wengi huvaa mashati ya zambarau siku ya Ijumaa. Anapendwa kiasi cha kwamba akisema anapenda rangi Fulani watu wake hubadilisha wanavyovaa.

Miaka kadhaa iliyopita jeshi limechukua dola Thailand. Kulikuwa na mapigano barabarani wafuasi wa serikali walipigana na wafuasi wa jeshi. Watu wote waliogopa hali itazidi kuwa mbaya. Halafu mfalme akasema. Aliwaambia waache kupigana na waandae uchaguzi. Mapigano yakaisha papo hapo. Hakuna wa kumhoji mfalme wote wakamtii. Haidhuru kwamba wamekuwa na hasira kiasi gani. Mfalme aliongea na kumfurahisha mfalme kumekuwa muhimu kuliko hisia zao.

Sisi tuna mfalme pia —Yesu ni mfalme wetu. Tusingepaswa kumfurahisha kama raia wa Thailand walivyomfanyia mfalme wao? Ikiwa wanaThailand wanampenda mfalme wao hadi kuvaa rangi anazozipenda si kweli kwamba maisha yetu yanapaswa kubadilishwa na upendo wetu kwa mfalme wetu Yesu?

Majadiliano ya wote

- Tunajitahidi kumfurahisha mfalme wetu katika mambo yote? Kwa nini tunafanya au hatufanyi?
- Kuna maeneo gani kwenye maisha yetu ambako tungeweza kujifunza kumtii Mungu vizuri zaidi?

Kutii kwa mambo yote

Mungu anataka tumfurahishe na tumheshimu muda wote. Soma Wakolosai3:17na 1Wakorinto10:31. Hapo tunaambiwa tumtukuze Mungu kupitia mambo yote. Mistari yote inasisitiza kwamba tumtukuze katika mambo yote. Wakolosai“Na **chochote** mnachokifanya ama kwa maneno ama vitendo, fanyeni kwa jina la Yesu mkimshukuru Mungu Baba kupitia kwake” ”Wakorinto“Kwa hiyo **mkila au kunywa au chochote mnachokifanya mfanye kwa utukufu wa Mungu**”Jambo linapojirudia kwenye biblia ina maana jambo hili ni muhimu. Paulo anataka tuelewe kwamba tunapaswa kumtukiza Mungu katika mambo yote.

Majadiliano ya wote

- Kwenye siku ya kawaida tunafanya nini na nini? (andika orodha ubaoni.)
- Tunawezaje kumtukiza Mungu tunavyofanya vitu hivi? (pitia orodha.)

Lazima tumtii mfalme wetu Yesu na tumfurahishe Mungu ametutendea mengi ametutumia mtoto wake. Tunapotafakari zawadi yake tunapaswa kuwa na nia kutii amri zake.

Kujenga ufalme wa Mungu

Soma Mathayo6:9-10

- Yesu anatuambia kuombea nini?
- Tutaonaje ujio wa ufalme?

Mungu anataka kujenga ufalme wake ulimwenguni. (Ufalme wako uje.)Ufalme wake hujengwa na watu duniani wanaofanya mapenzi yake. (Mapenzi yako yatimizwe.)

Kuna njia kuu mbili kujenga ufalme wa Mungu.Ya kwanza ni kuongeza idadi ya watu kwenye ufalme wake kwa kuhakikisha watu wanaokoka. Ya pili ni kuhakikisha kwamba mapenzi ya Mungu hutimizwa zaidi na zaidi na watu. Kama tulivyojifunza Yesu alikuja kupatanisha mambo yote (Wakolosai1:18-20).

Tukitaka mapenzi ya Mungu yafanyike inabidi kuwaona watu wengi zaidi wakiokoka na kumtii Mungu na tunahitaji kuwaona watu wengi zaidi kuishi kufuatana na mapenzi ya Mungu kwenye maeneo yote ya maisha yao.

Somo la 2 : Jamii za Ufalme

Lengo kuu

1. Kuelewa kwamba tukiwa watiifu wa kweli tutaona jamii yetu nzima inafanana na ufalme wa Mungu .

Vifaa

1. Kilichoandaliwa 2.1 hadithi za jamii
2. Karatasi kubwa
3. Penseli za rangi

Ufalme duniani

Unaweza kufikiria ufalme wa Mungu duniani unafananaje? Kwenye agano jibya tunaona mifano mingi jinsi wakristo wameungana kutengeneza ufalme wa Mungu duniani

Soma matendo ya mitume 2:42-47

- Waumini wapya wamefanyaje?
- Hivi ni vitu vya kimwili au kiroho? (vyote viwili)
- Matokeo yake yalikuwaje?
 - *hakuna mtu aliyekosa chochote, watu waliwapenda na wengine waliamua kuwa wakristo,*
- Tukiishi pamoja kama waumini wa kwanza tutaona nini kwenye jamii zetu?

Mungu kama kiongozi wa jamii zetu

Mungu anataka jamii zetu ziishi kama alivyotaka. Hataki tu mapenzi yake yatimie kwenye maisha ya mtu mmoja mmoja anataka yatimie kwenye jamii zetu pia.

KWENYE VIKUNDI VIDOGO

Maelekezo : Soma simulizi ifuatayo na ujibu maswali.(KILICHOANDALIWA 2.1)

Mwanamume fulani India alitembelea kijiji alipowahi kufanya kazi. Aliwauliza akina mama kijijini: je, ikiwa Yesu angekuwa kiongozi wao kijiji chao kingefananaje?. Umrai, mama mmoja jasiri alieleza kijiji chenye umoja na mshikamano. Alijua mgawanyiko kwenye kijiji chake haukuleta sifa kwa Yesu. Kila familia imejitegemea. Kutokana na jibu lake kikundi cha akina mama kijijini wakaunda kamati ya afya na kikundi cha kusaidiana. Wanawake ndani ya kikundi walikuwa watu kumi na nne wakaanza kukutana mara kwa mara wakiwa na moyo wa kushirikiana. Wanachama wakachanga hela kidogo kidogo na kuiweka kwenye akaunti ya pamoja na wakaanza kutatua matatizo ya jamii pamoja. Umrai alikuwa mwenyekiti wa kamati akatumiakipaji chake cha uongozi kupanga na kuhamasisha kijiji kufanya yale ambayo Yesu angalifanya angalikuwa kiongozi.

Akina mama wanachama wa kikundi cha Biblia Uganda wameamua kuhudumia kijiji kama Yesu angekuwa anawahudumia. Wamepanga mradi wao wa kwanza kwa umakini mkubwa. Mradi ulikuwa kuondoa taka kwenye eneo la baa. Wanawake wawili waliingia baa bila kuogopa. (Kwa kawaida wamama wanaoingia baa ni malaya tu) Wakaomba ruhusa kuondoa taka. Wenye baa wakacheka lakini wakakubali. Wanawake wakahamasisha jamii na watu wengi wakajitolea. Wakachimba mashimo mawili: moja kwa ajili ya taka zinazooza na jingine kwa ajili ya taka zisizooza. Wenye baa walipowaona wakaanza kuwasaidia Wakaendelea kuweka eneo lao safi na jamii ikafurahi.

Baada ya kutiwa moyo wanawake wakaamua kutengeneza majiko tisa zisizotumia kuni/mkaa nyingi kwa ajili ya familia kijijini kwao na pia kutoa vyombo vya kutunzia maji kwa wanaohitaji. Baada ya hapo kikundi cha kujifunzia biblia wakaanzisha mradi mkubwa zaidi: soko la jamii. Kwa kawaida wanawake kijijini hutembea masaa mengi kupeleka mboga na bidhaa kwenye masoko ya mbali. Soko lililo karibu lingewawezesha kupata mapato wakiwa karibu na familia zao, jamii na bustani zao. Wakapewa ardhi lakini ilikuwa na mtereremko mkali kwa hiyo hakufai kujengea soko. Wanawake wa kikundi cha biblia wakaomba na wafanyakazi wa barabara kuu waliotengeneza barabara karibu na kijiji wakajitolea kuja wakasawazisha eneo la soko bila malipo. Kwa msaada wa Mungu kikundi kidogo cha wanawake wa kikristo wakagundua na kukusanya rasilimali, wakaokoa pesa wakatatua matatizo na wakajenga soko la jamii. Maisha yao la kiroho yamekua huku wakiwahudumia wengine kwa niaba ya Yesu.

Jadili

- Nini kimetokea kwenye kila simulizi?
- Kutokana na watu kwenye simulizi hilo jamii zimeanza kufanana na jinsi maisha yalivyo ikiwa kila mmoja anaishi sawasawa na mapenzi ya Yesu ? Kwa nini?
- Taja baadhi ya mambo yaliyofanywa na watu kwenye simulizi hizo?
- Ungewezaje kufanya kitu kama hicho kwenye jamii yako?

Yesu ni kiongozi wa jamii

Majadiliano ya wote

Fikiria Yesu angekuwa kiongozi wa jamii yako. Kitu gani angebadilisha mara moja?

Maelekezo: Ikiwa kundi linafikiria tu kubadilisha viongozi wa kisiasa uwakumbushe kwamba Yesu alipokuwa duniani hakubadilisha viongozi. Wafuasi wake walitegemea angepindua utawala lakini hakufanya hivyo. Aliwabadilisha mtu mmoja mmoja. Kwenye programu hii tunalenga kuishi kulingana na mapenzi ya Mungu na kuwasaidia wengine wafanye hivyo hivyo.

Ikiwa kundi linapata shida kujibu utumie maswali kuchokoza majadiliano:

- Yesu angefanyaje kuhusu wajane na yatima?
- Angejengaje familia?
- Angefanyaje kupata maji salama nyumba nzuri chakula huduma za afya uondoaji wa taka na maji machafu na barabara nzuri?
- Angefanyaje kuhusu elimu ya watoto na watu wazima?
- Angefanyaje kuhusu ulevi wa pombe, madawa ya kulevya bahati nasibu na mengineyo?
- Angefanyaje kuhusu ukatili dhidi ya wanawake na watoto?
- Angeboreshaje mahusiano?

Kubadilisha jamii kwenye maeneo manne

- Unakumbuka njia nne ya kukua kama Yesu alivyokua? (Luka2:52)
 - busara, kimwili,kijamii na kiroho

Ufalme wa Mungu unaleta mabadiliko kwenye maeneo yote manne. Tukitaka jamii zetu zifanane na ufalme wa Mungu inabidi tufikirie mabadiliko kwenye maeneo yote manne kwenye jamii zetu.

vikundi vidogo

Maelekezo: Ugawe darasa kwenye vikundi na uwaambie wajaadili jamii bora ingefananaje? Uwaambie wafikirie maeneo ya kiroho, kimwili kijamii na kiakili. Uwaambie wachore picha kuonesha jinsi Mungu angependa maisha ya jamii yaweje.

Eleza:

Mungu anatamani jamii zibadilike zifanane na ufalme wake Alitulia moyo tuombe ufalme wake uje duniani kama uko mbinguni na alituambia tutafute kwanza ufalme wake.

Unaweza kufikiria kuishi kwenye jamii ambayo kila mmoja anamtii Mungu? Kungekuwa na familia zenye furaha, majirani wema wanaosaidiana na kuishi kwa amani. Kusingekuwa na ugomvi wala uwongo. Ungependa kuishi kwenye jamii ya aina hii?

Mungu analeta ufalme wake kupitia sisi. Tutasoma zaidi kwenye somo la 4 kwa sasa tufikirie: *(uzipitie polepole watu wawe na muda wa kufikiria.)*

- Ingekuwaje ikiwa kuanzia kesho saa 12 asubuhi wanakanisa wote wangeishi kufuatana na mapenzi ya Mungu?
- Sisi tungepatwa na nini tungemtii Mungu kuhusu mahusiano yetu utunzaji wa mmiili yetu na kuishi kwetu na Mungu?
- Ikiwa wote tungetii malengo ya Mungu kuhusu mahusiano yetu familia zetu zingekuwaje?
- Mekanisa yetu yangukwaje kama viongozi na waumini wangependana wangehudumiana wangependana wadhaifu na masikini na wangeishi kwa umoja?

Mungu ametupa maono: maono ya ufalme wake duniani. Anataka tushiriki kuujenga. Fikiria kila mtu angemtii Mungu Ingekuwa kama tuko mbinguni. Pamoja na kwamba hayatakamilika hadi Yesu atakaporudi tunaweza kuanza kutekeleza maono hayo yatokayo kwa Mungu.

Kila siku tuamke tujiulize leo nitajengaje ufalme wa Mungu. Nitaikuzaje ufalme wa Mungu? Nitaishije kufuatana na sheria za Mungu? Nitaaidiaje familia yangu wafanye vivyohivyo?

Somo la 3 : MAADILI YA UFALME

Malengo makuu

1. Kuelewa kwamba matatizo kwenye jamii zetu yanaweza kutatuliwa tu ikiwa tunamtii Mungu kikamilifu.
2. Kuona kwamba ufalme wa Mungu unakuja tunapotekeleza Biblia kwenye kila eneo la maisha yetu.
3. Kuona kwamba kanuni za biblia ziko tofauti na maadili ya jamii zetu
4. Kuelewa kwamba tunaelewa kanuni za biblia tunapoisoma

Vifaa

1. kilichoandaliwa 3.1 Karatasi ya maadili ya ufalme
2. Somo la 3: Mabango yenye kanuni za msingi

Kanuni za msingi

Tuangukie kanuni tatu za msingi.

Dunia imeharibika. Busara na vifaa vya wanadamu haviwezi kuponesha dunia.

- Utoe mifano ya matokeo ya dhambi duniani
majibu
 - *ulevi/bahati nasibu/umalaya*
 - *familia zilizoharibika*
 - *ugomvi*

Soma simulizi lfuatayo:

Taifa la Haiti ni mfano wa yaliyo haribika bila kutengenezwa kwa busara au vifaa vya kibinadamu. Haiti ni nchi masikini zaidi Amerika ya Kati na Amerika Kusini. Ina watu milioni 8. Tangu 1980, maelfu ya programu ya kimataifa ya kiserikali na zisizo za kiserikali zimetekelwa. Mabilioni ya dola za kimaerikani zikatumika kuboresha hali ya kiuchumi, kijamii na kiroho ya Haiti. Hata hivyo hakuna kilichobadilika. 2004 mashirika na serikali za kimataifa zikatoa tena bilioni 1 ya dola za kimaerikani kutatua matatizo ya Haiti.

Pamoja na hela zote hizo Haiti haijabadilika. Watu wanateseka bila matumaini. Asilimia 80 ya watu ni masikini sana. Nchi haina viwanda na hakuna biashara. Asilimia 70 ya watu hawana kazi. Asilimia 10 ya watoto wanakufa kabla hawajafikia miaka minne. Makazi holela yamejaa watu, hakuna nyumba nzuri, uchafu umezidi na uhalifu umezidi. Barabara zimeharibika na hakuna maji ya kutosha. Kijijini kwenyewe hakuna unafuu. Baada ya miaka mingi ya kukata miti ovyo vijiji havina ardhi nzuri na vinapigwa na upepo mkali mara kwa mara.

Pamoja na fedha zote na mawazo ya mabingwa hakuna mabadiliko. Nchi haikuponeshwa kupitia fedha wala ushauri wa mabingwa duniani.

- Haiti kuna hali gani?
- Fedha ngapi zikatumika Haiti?
- Matokeo yake yalikuwaje?
- Kwa nini ilikuwa hivyo?

Dunia imeharibika na mawazo yetu mazuri hayatoshi kuitengeneza. Hiyo ni kweli kote kote si Haiti tu. Hata bara la Afrika bado kuna umasikini pamoja na misaada na mabingwa wote. Busara ya kibinadamu na vifaa havitoshi kuponesha dunia. Tunahitaji kitu cha ziada.

Taifa linapona pale ambapo watu wanamwitikia Mungu na wanaishi anavyoelekeza yeye.

Soma 2 Nyakati 7:14

- Biblia inasema tufanyaje?
- Nani anapaswa afanye—Wakristo au wasio Wakristo?
- Tunapofanya mambo haya kutatokea nini ?
- Unaamini mstari unasema ukweli?
- Tukitaka jamii yetu ipone tufanyaje?

Mungu anataka jamii zetu zipone. Yesu amekuja kupatanisha mambo yote. Kwa sasa anafanya kazi kupitia sisi. Bila maombi yetu kufunga kwetu na utiifu wetu kwa Mungu hakuna uponaji! Uponaji wa jamii zetu huja tunapofanya mambo hayo. Unataka jamii yetu ipone? Uko tayari kufanya mambo hayo?

Biblia inatuambia namna ya kuishi kuponesha taifa letu na kujenga ufalme wa Mungu.

Mara nyingine tunaponunua kitu cha thamani tunapewa kijitabu kutuonesha jinsi ya kuitumia. Kijitabu kimeandikwa na kampuni iliyobuni na kutengeneza bidhaa hiyo. Wanajua namna ya kuitumia ili ifanye kazi vizuri na kwa muda mrefu zaidi. Tukitaka matokeo bora kutokana na bidhaa lazima tusome kijitabu hiki.

Ndivyo Mungu alivyo. Alitengeneza dunia na alitutengeneza sisi. Anajua namna ya kuboresha dunia na maisha yetu. Na alituandikia kitabu. Kinaitwa Biblia. Humu anatuelekeza jinsi ya kuishi kwenye kila eneo la maisha yetu. Biblia ina maelekezo na busara yote ya kuponesha dunia na jamii zetu zilizoharibika. Tunapaswa kusoma, kuelewa na kutekeleza kilichoandikwa kwenye kila eneo la maisha yetu tukitaka maisha bora na mabadiliko kwenye jamii zetu.

Maelekezo: Kwa kutumia kadi urudie tena dhana zote tatu. Uhakikishe darasa linaelewa kila kadi.

- Tumejifunza nini kuhusu kuponesha dunia yetu?
- Tutawezaje kumtii Mungu?
 - Lazima tusome Biblia na tuitumie kwenye kila eneo la maisha yetu.
- Mungu ametuahidi nini tukiwa tunamtii?

Kutekeleza biblia kwenye kila eneo la maisha yetu

Ukisoma maisha ya Yesu duniani utakuta wafuasi wa Yesu walitofautiana na yeye kuhusu anavyopaswa kutawala.

Soma Marko 10:35-37, 41-45

- James na Yohana wamejadili nini?
- Yesu alisemaje kuhusu kiongozi anvyopaswa kutenda?

James na Yohana walifikiria kimila. Walitaka kuwatawala wengine na walifikiria kuwa viongozi. Lakini Yesu aliwasahihisha akawaambia kwamba kiongozi mkuu ni mtumishi.

- Unaona mtumishi ameishije enzi zile?
- Walipoambiwa hivyo wafuasi wa Yesu watakuwa wamejisikiaje?

Mara nyingi mambo yako hivyo. Njia ya dunia njia ya mila si njia za Mungu. Tukitaka kujenga ufalme wa Mungu duniani lazima tujue njia zake. Mungu ametupa Biblia inayotunesha jinsi ya kuishi ili tumpendeze Mungu

Kwenye vikundi vidogo

Jaza jedwali lifuatalo (kilichoandaliwa 3.1). Kwa kila kipengele ufikirie mila yao inavyosema halafu angalia mistari uone Biblia inatuambia tufanyaje.

<i>maadili</i>	<i>maandiko</i>	<i>Mila zetu/ desturi</i>	<i>Ufalme wa Mungu</i>
<i>Tuwe na tabia gani kama mume</i>	<i>Wakolosai 3:19 1 Petro 3:7 Waefeso 5:25,28,33</i>		
<i>Tuwe na tabia gani kama mke</i>	<i>Kitabu cha Mwanzo 2:18 Waefeso 5:22-24,33</i>		
<i>Namna ya kukaa na watoto</i>	<i>Zaburi 127:3 Waefeso 6:4</i>		
<i>Namna ya kukaa na watu</i>	<i>Mathayo 22:36-40</i>		
<i>Namna ya kuishi na maadui</i>	<i>Luka 6:27-31</i>		
<i>Mtazamo wetu juu ya kazi</i>	<i>Wakolosai 3:22-4:1 Waefeso 6:7-8</i>		
<i>Mtazamo wetu juu ya mazingira</i>	<i>Zaburi 24:1 Mwanzo 1:28-30 Mwanzo 2:15</i>		
<i>Kitu chenye muhimu zaidi</i>	<i>Mathayo 6:25-34 Mathayo 22:36-40</i>		
<i>Mtazamo wetu juu ya kifo na kufa</i>	<i>Yohana 11:25-26 Waebrania 2:14-15 Ufunuo 1:17-18</i>		
<i>Mtazama wetu juu ya kuteseka</i>	<i>Luka 6:22-23 2 Wakorinto 1:8-11</i>		

Tafuta kanuni za Mungu

Wiki hii unaposoma Biblia utafute kanuni za Mungu uzitekeleze kwenye maisha yako. Unaposoma sura au sehemu ujiulize maswali yafuatayo:

- Hapo najifunza nini kuhusu Mungu?
- Hapo nafundishwa nini kuhusiana na ninavyopaswa kuishi?
- Hapo ninafundishwa nini kuhusiana na mahusiano?
- Hapo ninafundishwa nini kuhusu utunzaji mazingira, ninavyopaswa kufanya kazi au ninavyopaswa kutumia pesa?

Somo la 4: Maadili ya ufalme na kazi

Malengo makuu

1. Kazi ni eneo muhimu kwenye maisha yetu ambapo tunaweza kuleta utukufu kwa Mungu. Biblia inatuonesha jinsi ya kutii kazini na jinsi ya kufanya kazi ili tumtukuze Mungu.

Vifaa

1. Kilichoandaliwa 4.1 mwongozo wa majadiliano kwenye kikundi kidogo
2. Somo la 4 Mwongozo wa John Wesley wa kazi

Utangulizi

Majadiliano ya kundi kubwa

- Kazi ni kitu kizuri au kibaya ?
- Kwenye lugha yako kuna methali gani zinazohusiana na

kazi ? Mwanzo1:28

- Maagizo ya kwanza ya Mungu kwenda kwa Adamu yamesemaje ?
- Hayo yalitokea kabla au baada ya Adamu kula tunda?

Mwanzo2:2

- Mungu anapumzika baada

ya kufanyaje? Marko6:1-3

- Yesu alikuwa na kazi gani kabla hajaanza kufundisha?

Kama tunavyoona kwenye mistari hii Mungu amefanya kazi na sisi tumeumbwa kufanana na Mungu. Toka mwanzoni kabla ya dhambi kutokea binadamu alikuwa anafanya kazi.

Kwenye kitabu cha Ruthi, tunajifunza historia ya Ruthi. Anakimbia njaa na mama mkwe wake na yeye ni masikini sana. Wanarudi Moab baada ya kusikia kwamba pale kuna chakula. Ruth anapata kazi kwenye shamba la Boaz, Boaz anavutiwa na Ruthi na anapata habari alichomfanyia mama mkwe wake.

- Boas amefanyaje kumsaidia Ruthi? (Ruth2:15-16)
- Kwa nini hakumpa ngano moja kwa moja?
 - *Tumeumbwa kufanya kazi kwa hiyo heshima yetu hutokana na kazi sivizuri kupokea msaada tu. Boaz alimheshimu Ruthi ndiyo maana akampa kazi si msaada.*

Mtazamo wa kibiblia juu ya kazi

Kwenye vikundi vidogo

Jadili ukitumia kilichoandaliwa 4.1. Sababu za kufanya kazi ni zipi? Utumie mistari ifuatayo na mawazo yako kwenye kipindi.

- 1Wathesaloniki e 4:11-12
- 1Timotheo 5:8
- Waefeso 4:28
- 1Wakorinto 10:31

Majadiliano ya kundi kubwa

- Unadhani Mungu anataka tufanye kazi?
- Kwa kawaida watu wanaionaje kazi?
- Mungu alipopanda bustani na Yesu alipokuwa fundi seremala unadhani walikuwa na mtazamo gani kuhusu kazi ?
- Tutawezaje kuwa na mtazamo unaofanana na mtazamo wa Mungu?
- Tutawezaje kuwasaidia wengine kuwa na mtazamo wa kiMungu kuhusu kazi zao?

Mtu mmoja mmoja

- Una mtazamo gani kuhusu kazi yako?
- Unapaswa kubadilisha mtazamo wako?

Umwombe Mungu uone kazi yako kupitia macho yake na akupe mtazamo unaofanana na ya kwake.

Aina za kazi

Majadiliano ya kundi kubwa

- Unafikiri kuna kazi zilizo muhimu kuliko zingine? Kwa nini zinakuwa muhimu zaidi?

Kwenye vikundi vidogo

- Mungu alimpa Adamu kazi gani?
- Mungu alimpa Nuhu kazi gani?
- Mungu alimpa Yusufu kazi gani?
- Mungu alimpa Danieli kazi gani?
- Mungu alimpa Gideoni kazi gani?
- Mungu alimpa Musa kazi gani?
- Mungu alimpa Daudi kazi gani?
- Unafikiri Mungu angefurahia zaidi ikiwa watu hawa wangeongoza kanisa na kuhubiri badala ya kufanya zile kazi alizowapa?
- Unafikiri Mungu aliwaona watu wake hao kutokuwa na umuhimu sawa na makuhani? Kwa mfano kazi ya Aron ilikuwa muhimu kuliko kazi ya Musa?

Biblia haitofautishi kazi muhimu na zisizo muhimu. Kuona kazi Fulani kuwa muhimu na nyingine si muhimu dhana inayotokana na mila za kigriki na hadi Mageuzi kanisani dhana hiyo iliingia kwenye Ukristo pia. Wagiriki waliamini mambo ya kiroho ni muhimu kuliko mambo ya kimwili.

Hata hivyo mtazamo huo si mtazamo wa Biblia. Biblia inaanza na Mungu akiumba ulimwengu. Mwanzo 2:8 tunamwona Mungu akipanda bustani. Mungu tunayemsifu amepanda bustani. Tunapofanya kazi shambani tukumbuke Mungu alikuwa mkulima wa kwanza. Tunafanya alivyofanya Mungu zamani. Mungu aliwaita watu mbali mbali kwa kazi tofauti tofauti. Kuwa mchungaji au mwinjilisti ni kazi nzuri sawa sawa na kulima, fundi seremala au kufundisha. Hatuhitaji walimu wa kiroho tu mbali tunahitaji wanaolima chakula, wanaojenga nyumba, na wanaowafundisha watoto wetu. John Wesley, mkristo maarufu aliyeishi miaka 200 iliyopita alitoa mwongozo ufuatao wa kazi.

Mwongozo wa John Wesley (Picha2)

- Kazi isiathiri afya yako
- Kazi isiathiri familia yako
- Kazi isiende kinyume na dhamira yako
- Kazi isiathiri jirani yako au uwezo wake wa kupata pesa kupitia kazi zake
- Kazi isiathiri mwili wa mwenzako
- Kazi ismfanye mwenzako atende dhambi.

John Wesley alisema kwa kuzingatia mwongozo huo tutumie vipaji vyetu kufanya kazi kwa kadiri ya uwezo wetu. Lazima tupate pesa ya kutosha kutunza familia zetu, weka akiba ya baadaye, ya kutoa kwa ajili ya kuendeleza kazi ya Mungu na kuwasaidia masikini. Tunapofanya hivyo tunamheshimu Mungu kwa kutumia vipaji wetu nguvu na afya alizotupa.

Majadiliano ya kundi kubwa

Angalia mwongozo wa John Wesley

- Toa mifano ya hali inayopingana na muongozo huo?
 - o *Kazi isiathiri afya yako— kufanya kazi kwenye mazingira hatarishi kazi inayopingana na hali yako kwa mfano kazi ngumu kwa wazee*
 - o *Kazi isiathiri familia yako— kufanya kazi masaa mengi kiasi cha kwamba huonani na familia yako. Kuwa mbali na familia yako kwa wiki nyingi ndani ya mwezi.*
 - o *Kazi isiende kinyume na dhamira yako—kuiba au kumwonea mtu.*
 - o *Kazi isiathiri jirani yako au uwezo wake wa kupata pesa kupitia kazi zake—kuanzisha biashara sawa na jirani yako na kuuza kwa bei ya chini zaidi ili upate wateja wake*
 - o *Kazi isathiri mwili wa mwenzako— kutengeneza pombe au sigara*
 - o *Kazi isimfanye mwenzako atende dhambi— kuendesha baa.*
- Tukiamini kila kazi inaleta utukufu kwa Mungu utaonaje kazi yako?
- Inabadili unavyofanya kazi yako?

Mungu anajali tunavyofanya kazi

Mara nyingi inasemekana wakristo ni wafanya kazi wabaya kabisa

- Kwa nini hiyo ni kweli?
- Hayo hutokea kwenye eneo lako?
- Mungu anajisikiaje juu ya sifa hiyo?

Biblia haisemi kuna kazi zisizo muhimu lakini inatuelekeza kwa undani jinsi ya kufanya kazi. Kazi ni sehemu muhimu ya kila siku. Tunatumia masaa mengi zaidi kwenye kazi kwa hiyo ni muhimu kutafakari namna ya kufanya kazi.

Kwenye vikundi vidogo

Soma mistari ifuatayo. Mistari hii inafundisha nini juu ya kazi? Kwenye vikundi vidogo utoe muhtasari wa sentensi moja.

- 2 Wathesalonike 3:10-12
- Mithali 10:4
- Mithali 19:15
- Mithali 21:25

Mistari hii inafundisha nini kuhusu kazi?

- 1Wakorinto 10:31—kumtukuza Mungu
- Wakolosai 3:23—fanya kazi kama unamfanyia Mungu

Majadiliano kwenye kundi kubwa

Muda mrefu zaidi kwenye maisha yake Yesu alikuwa fundi seremala. Jaribu kufikiria ungalimwona akiwa fundi.

- Ubora wa kazi yake ulikuwaje?
- Ingekuwaje kufanya kazi naye?
- Angekuwa na tabia gani?
- Anapokuwa peke yake angefanyaje?

Wakati wa Mageuzi kanisani kazi ya Wakristo ilibadilika mno. Kwa mara ya kwanza wakristo wamesoma biblia. Wakati ule seremala akitengeneza meza aliweka mapambo hata chini ya meza akijua Mungu anaona kote kote juu na chini, nje na ndani na fundi alitaka kumfurahisha Mungu na kazi yake. . Enzi zile watu walitengeneza vitu vyenye uzuri wa aina yake.

Kwenye vikundi

Vidogo

Maigizo

Chagua kazi halafu mwigize mtu mmoja anayemfanyia kazi Mungu na yule ambaye hamfanyii kazi Mungu. Mtoe igizo lenu mbele ya washiriki wote.

Kundi kubwa

Mjadili baada ya kila igizo:

- Aliyemtukuza Mungu kupitia kazi yake alitumia njia zipi?
- Asiyemtukuza Mungu naye alitumia njia zipi?
- Kuna njia zipi zingine za kumtukuza/kutokumtukuza Mungu?

Tafakari

Fikiria kazi yako. Unamtukuzaje Mungu kwenye kazi yako. Mwombe Mungu akuoneshe jinsi utakavyoweza kumtukuza zaidi.

Somo la 5: Kujenga Ufalme wa Mungu

Malengo makuu

1. Lazima tuwe watiifu kwenye maisha yetu binafsi na kwenye maisha yetu ya familia ili kubadilisha jamii zetu zifanane na Ufalme wa Mungu.

Vifaa

1. kilichoandaliwa 5.1 'Familia moja ya kikristo inaleta tofauti' simulizi
2. kilichoandaliwa 5.2 NAMNA YA KUWA MJENZI WA UFALME
3. Picha Somo la 5 – mtu mmoja hadi familia

Inaanzia kwetu

Kwenye somo la kwanza tumezungumzia jinsi Mungu ametupa maono ya ajabu.

- Maono yalikuwa maono gani?
 - *Ufalme wa Mungu*
- Tufanyaje kutekeleza maono hayo?

Jamii iliyobadilishwa

Soma simulizi ifuatayo.

Kulikuwa na eneo ambako wakristo walikuwa masikini sana kwa miaka mingi. Familia nyingi zilikuwa na pato la chini. Walipanda mashamba ya mbali wakabeba mazao yao mgongoni kwa sababu barabara ilikuwa mbaya sana na magari yasingeweza kupita. Familia nyingi walipata chakula cha kuwatosheleza miezi 6 tu. Miezi 6 iliyobaki waliingia msituni kutafuta chakula. Kwa sababu hawakujua kutunza bajeti familia zikapata madeni kila mwaka. Jamii ilikuwa haina vyoo na watu waliumwa mara kwa mara. Nyumba zao zilikuwa ndogo sana na zilikuwa zinavuja. Watoto hawakwenda shule kila siku Kanisa lenyewe lilikuwa dogo sana wakateswa na kugombana wao kwa wao.

Mashirika ya maendeleo hayakuruhusiwa kufanya kazi nao na kwa hiyo hakukuwa na matumaini ya mabadiliko. Hali hii imebadilika baada ya familia moja kuja na kuwafundisha baadhi ya viongozi wa kanisa kuhusu kumpenda jirani yako na maana ya ufalme wa Mungu. Hawakuwapa makanisa pesa yoyote waliwafundisha tu viongozi maana ya kutii amri za Mungu.

Makanisa yameitikia kwa kuwasaidia watu wengine kwenye jamii. Walitengeneza na kuzipanua barabara. Walisaidiana kuvuna. Walijenga na kuzitengeneza nyumba. Walijenga vyoo. Waliwapeleka watoto shule. Waliwaheshimu wake/waume zao.

Ndani ya miaka mitano jamii imebadilika kabisa ! Viongozi walikuja wakatoa taarifa. Jamii hazikuwa maskini tena. Mapato yameongezeka, walikuwa na afya bora, watoto wakaenda shule. Tena makanisa yamekua pia! Karibu kila mtu amekuwa mkristo baada ya kuona upendo wa Mungu kwenye jamii. Kanisa lilijenga mahusiano mazuri na serikali kwa hiyo halikufuatiliwa tena.

Walipokuja wakristo wageni kutoka shirika fulani la maendeleo kuona kilichotokea hawakuamini kwamba jamii walikuwa masikini hapo awali. Walipoona jinsi jamii ilivyobadilika ndani ya miaka mitano tu walishangaa. Wakamwuliza kila kiongozi umefanyaje kuleta mabadiliko hayo.

Unajua viongozi walisemaje? Kila mmoja alitoa jibu lile lile: Tulimtii Mungu.

Majadiliano ya kundi kubwa

- Kitu gani kimebadilika kwenye jamii hii?
- Mabadiliko hayo yahasu mambo ya kiroho au mambo ya kimwili?
- Wafanyakazi kutoka shirika la maendeleo walipoulizia jamii imefanyaje ili wabadilike unafikiri walitegemea kupata jibu gani?
- makanisa kwenye jamii yalifanyaje kuonesha utiifu wao kwa Mungu?

Tunaibadilishaje jamii yetu?

Tukitaka kuona jamii yetu inabadilika inabidi tumtii Mungu. Hatua ya kwanza ni kubadilisha maisha yetu sisi wenyewe. Lazima tuzingatie maadili ya ufalme kwenye kila eneo la maisha yetu.

Majadiliano ya kundi kubwa

- Maisha yetu yangekuwaje tungemtii Mungu kila dakika kila siku?
- Ufikirie unayoyafanya kila siku. Ungemtii Mungu ungefanya hivyo? Ungezifanya kazi kwa namna tofauti?
- Mapenzi ya Mungu yanahusikaje na vitu vya kawaida kama kulala, kula, kupika, kulima au kuteka maji? Mungu anajali tunavyovifanya vitu hivi?
- Soma Mathayo 6:25-33
 - Watu walifikiria nini? Vitu hivi ni vya kiroho au vitu vya kawaida?
 - Yesu alijibuje?
 - Yesu alimaanisha nini? Tutawezaje kutafuta ufalme wa Mungu katika mambo yote?

Inachanganya kusikia kwamba walipofikiria chakula Yesu aliwaambia tafuteni kwanza ufalme wa Mungu. Msemo huu unamaanisha nini? Unamaanisha tuombe tu tusifikirie vitu hivi? Tukifanya hivyo maisha yangekuwa mazuri?

Kwa bahati nzuri kwetu kulikuwa na MTU aliyeishi maisha kamilifu. Alitenda mapenzi ya Mungu muda wote: Yesu(Yohanna14:31).Tunaweza kufuatilia maisha yake ili tuelewe maana ya kutafuta kwanza ufalme wa Mungu. Soma mistari ifuatayo inatufundisha nini kuhusu alichokifanya Yesu?

- Marko 6:3–hadi alipotimiza miaka 30 Yesu alikuwa fundi seremala. Kwao walimwona kama mtu wa kawaida si kama kiongozi wa kiroho. Wakati alipokuwa fundi aliishi maisha kikamilifu. Hakuna dakika alipokuwa nje ya mapenzi ya Mungu. Kuanzia miaka 10 hadi 30 Mungu alitaka Yesu afanye kazi ya familia yake awe fundi seremala.
- Yohana 21:9-14–Yesu aliwapikia wafuasi wake.
- Marko 4:38–Alipochoka Yesu amepumzika
- Yohana 2:1-2–Yesu alihudhuria arusi.
- Hivi vitu vilikuwa vitu vya kawaida au vilikuwa vya kiroho?
 - Vilikuwa vitu vya kawaida na Yesu alitumia muda wake kuvifanya. Alikuwa akitafuta ufalme wa Mungu huku akifanya vitu vya kawaida. Hakwenda nje ya mapenzi ya Mungu bali alitimiza mapenzi ya Mungu kikamilifu.

Soma Marko1:21-34

- Yesu amefanya nini siku ile?

Hapo tunaona Sabatho kwenye maisha ya Yesu. Asubuhi alifundisha kwenye Sinagogi halafu alienda kwenye nyumba ya Peter, baada ya kumponesha mamake Peter Yesu alipumzika huku akihudumiwa na mamake Peter. Jioni alitoka kuwasaidia wengine akiwaponya wagonjwa.

- Kuna tofauti gani kati ya jumapili zetu na sabatho ya Yesu? Nini ni tofauti nini inafanana?

Kama tunavyoona mwanzo wa maisha yake Yesu alikuwa fundi seremala. Hata alipoanza kufundisha hakutumia muda wote kuomba na kufundisha. Alikula na marafiki aliwahudumia marafiki alilala na kupumzika. Yote aliyoyafanya yalikamilika na yaliendana na mapenzi ya Mungu. Hata alipofanya vitu wa kawaida alifanya kutokana na yale ambayo Mungu alitaka afanye.

Bruda Laurensio

Mnamo mwaka 1608 mtu amezaliwa Ufaransa. Alipokuwa na miaka 18 alikuwa mkristo na alipofikisha miaka 20 aliamua kumtolea Mungu maisha yake. Aliingia kwenye nyumba ya mabruda akapewa jina la Bruda Laurensio. Alifikiri atatumia maisha yake yote kanisani akiomba na kumsifu Mungu. Hata hivyo alipangiwa jikoni. Kwa miaka 10 alichukia kuwa jikoni wakati wenzake wako kanisani. Hakutaka kupewa kazi hizo zisizo za maana.

Majadiliano kwenye vikundi vidogo


- Ungalikutana na Bruda Laurensio wakati ule ungalimshaurije?
- Unafikiri mabruda kanisani walikuwa na kazi muhimu kuliko kazi ya Laurensio?
- Usume mistari ifuatayo mistari hiyo inahusikaje na maisha ya Laurensio?:
 - Mathayo 25:40(34-40)
 - 1 Wakorintho 10:31
 - 1 Wakorintho 13:1-3

Baada ya miaka 10 Bruda Laurensio aligundua kwamba anaweza kumhudumia na kumsifu Mungu popote aliko. Alibaki jikoni lakini alisikia uwepo wa Mungu jikoni sawasawa na kanisani.

Biblia inatuonesha Mungu anajali zaidi tunavyofanya tunachokifanya chochote huweza kuleta utukufu kwa Mungu.

Kutoka Familia hadi jamii

Mabadiliko yaaanzia kwa mtu halafu yanafikia familia halafu jamii halafu taifa. Huo ni mchakato. Watu na familia zinapomtii Mungu jamii hubadilika. Jamii moja hubadilisha nyingine hadi taifa lote linabadilika.



Familia

Soma mistari ifuatayo;

- Kumkumbu la torati 6:7
- Tito 2:3-4
- 1Timotheo 3:12
- Tito 1:6
- Tunapaswa kuzibadilishaje familia zetu?
 - Lazima tuwafundishe na kuwapa mfano bora.

Soma Luka 2:52

- Tumejifunza nini kutokana na mstari huo kwenye mafunzo yaliyopita?
 - Lazima tukue kwenye maeneo yote manne.

Kwenye vikundi vidogo

Utafute njia nyingi iwezekanavyo kuwafanya wanafamilia wako wakue katika maeneo yote manne. Kila mmoja achague kitu kimoja atakachokifanya kwenye kila eneo (kijamii, kiroho, kimwili na kiakili) wiki hii.

Jamii

Familia zikishabadilika hutaka kubadilisha jamii. Soma simulizi ya mtu na familia yake walipobadilisha jamii (Kwa wanaojua kusoma uwape kilichoandaliwa 5.1 na uwaambie wasome wenyewe.)

Hili ni simulizi ya kweli kuhusu mtu aliyehamia na familia yake kwenye eneo lisiilokuwa na wakristo kuwapa habari ya Kristo. Alitaka kuona ufalme wa Mungu ujengeke na watu wabadilike kwenye kila eneo—kiroho, kijamii, kiakili na kimwili.

Familia moja ya kikristo huleta tofauti

Miaka minne iliyopita mwinjilisti alipohamia hapa jamii yote walikuwa wahindu, kijiji kiko Himalaya 1,000ft. juu kutoka usawa wa bahari. Kilometa chache kutoka kijijini kulikuwa na shamba la chai. Huku ndiko wanakijiji wengi walipofanya kazi, Hata hivyo mishahara ilikuwa midogo na kwa hiyo watu walihangaika hata kama walikuwa na kazi.

Kijijini kulikuwa na nyumba ishirini na tano zilizojengwa kwa mbao na kuezekwa kwa mabati. Hakukuwa na vyoo. Kwa sababu kulikuwa juu sana kulikuwa na baridi kali lakini watoto walikuwa hawana viatu pia walikuwa na utapia mlo.

Kila nyumba imejengwa kwenye eneo dogo la ardhi. Kulikuwa na kibanda kilichojaa moshi karibu na kila nyumba humu wamepika kwa kutumia mafiga. Kulikuwa na kuku wachache waliokimbia ndani na nje ya nyumba. Nyua zimekuwa chafu.

Shule ilikuwa kwenye umbali wa kilometa mbili ilikuwa mbali sana kwa watoto kutembea kila siku na

pia walitakiwa kufanya kazi karibu na nyumbani. Kwa hiyo watoto wengi hawakuenda shuleni Watu wazima wengi hawakuweza kusoma na kuandika kwa hiyo walinyanyaswa na wanavijiji kutoka vijiji vingine waliojua kusoma na kuandika.

Kulikuwa na bustani chache kwa sababu maji yalipatikana kwenye umbali wa kilomita 2 kwenye bwawa. Ilikuwa ngumu kupata maji kwa ajili ya kunywa na kuoga bila kufikiria kuleta maji kwa ajili ya kumwagilia bustani. Zamani kulikuwa na bomba kutoka kwenye bwawa lakini liliharibika na wanavijiji hawajalitengeneza bado.

Mvua ilikuwa ya shida isipokuwa kwenye msimu wa kulima mpunga. Wakati wa kulima mpunga hapakuwa na nafasi ya kulima mbogamboga. Wakiwa na bahati wanapata mpunga wa kutosha hadi msimu ujao.

Watu walikuwa wahindu waliabudu miungu mbalimbali. Kulikuwa na miungu mingi ambayo inabidi kuwaheshimu na kuwaabudu. Kijiji kilikuwa na miungu midogo mingi. Kila wanapokula wanakijiji hudondosha chakula kidogo kwa ajili ya mizimu.

Watu walikuwa wamekata tamaa. Tumaini lao ilikuwa kuzaliwa upya kwenye mazingira bora. Ila wangewakasirisha miungu wangeweza pia kuzaliwa upya wakiwa panya au mbwa. Walikuwa wamekata tamaa. Hawakuwa na namna ya kuboresha maisha yao.

Lepcha alikuwa mwinjilisti aliyehamia maeneo hayo. Alisoma kozi ya mwezi mmoja kuhusu kuwasaidia watu kuboresha afya zao. Baada ya kumaliza masomo hayo alihamia kijijini pamoja na familia yake ili wakae pale na kuwasaidia majirani kwa kuwashirikisha walichojifunza. Walikuwa na ua msafi na kibanda cha kupikia chenye jiko lililojengwa kuwa juu zaidi ili kurahisisha kupika. Pia jiko hilo limetumia kuni chache. Walikuwa na kibanda kidogo cha kuku. Walipanda bustani kuboresha lishe ya watoto. Walikuwa na choo cha nje na watoto wao hawakuwa na minyoo wala hawakuharisha mara nyingi kama watoto wengine kijijini.

Lepcha alitengeneza beseni la kukusanya mvua kutoka kwenye mabati wakati mvua ilinyesha. Wengine waliiga mfano wake na wakapata maji pia.

Waliwafanya watu washirikiane kuweka bomba kutoka kwenye bwawa hadi kijijini na sasa wanavijiji wana maji ya kutosha hata kwa ajili ya kumwagilia bustani zao mpya. Watu wengi waliiga banda la kuku na wakajenga vyoo.

Akina Lepcha walipokuja waliwafundisha watu wazima na watoto kusoma na kuandika. Walianza kuwafundisha watoto na vijana kusoma. Leo kijiji kina shule hadi darasa la nne. Sasa kuna kanisa dogo kwa sababu familia ishirini na tatu kati ya ishirini na tano wana mahusiano na Kristo. Yote hayo kwa sababu familia moja ilimtangaza Kristo kupitia maneno yao na vitendo vyao.

Watu wanajivunia mafanikio yao na wameona wanaweza kuishi maisha yenye afya kwa sababu familia moja iliwajali wakaja kuwashirikisha maisha yao.

Simulizi hiyo inajirudia rudia kwenye vijiji kaskazini ya India na Nepal mashariki. Leo mambo hayo yanajirudia kwenye vijiji 120 kwenye eneo hilo. Maisha ya watu yanabadilika lakini wanabadilika pia kiroho vikundi 107 vya maombi vilianzishwa. Na 12 vilivyo vikubwa zaidi vina wanachama 200.

Wachungaji wa India walianzisha dhehebu lao iitwayo kanisa la Agape Church makanisa hayo mapya

mengi zaidi yatajiunga na Kanisa hilo. Familia moja ya wakristo walipopata maono kubadili jamii yao wakitafuta mapenzi ya Mungu na kufuata maono waliyopewa na Mungu mambo makubwa yaliweza kutendeka. Baadhi ya mifumo inayotegemea familia imebadilishwa kuwa mifumo inayotegemea makanisa kwa kuwafundisha watu muhimu kanisani. Tunaomba huku mbele tuingie kwenye mifumo ya jamii.

- Kulikuwa na mabadiliko gani yaliyoletwa na Lepcha kwenye jamii? Pitia simulizi upya na utengeneze orodha ifuatayo: Mabadiliko ya kijamii, ya kiroho, ya kiakili, ya kimwili.
- Aliwezaje kuleta mabadiliko hayo? Alianza na nani? Familia yake
- Jamii imebadilikaje kutokana na Lepcha?
- Unaweza kuwa kama Lepcha kwenye jamii yako?

Kumbuka: *Kwenye awamu ya 4 tutakuletea mafunzo ya afya yanayofanana na yale aliyoyasoma Lepcha.*

Mifano mingine ya watu waliojenga ufalme wa Mungu

Soma simulizi zifuatazo mjadili maswali baada ya kila simulizi

Kusaidia hospitalini

Mchungaji kwenye nchi fulani alipeleka maandiko msikitini. Serikali haikufurahi hawakumruhusu kuendelea na kazi ya uwinjilisti. Siku moja alipitia mafunzo akifundishwa kuonesha upendo wa Mungu kupitia vitendo vya upendo. Alifikiria mpango mpya. Alitafuta wenzake wanne akanunua mkate na akaomba ruhusa kuwatembelea wagonjwa hospitalini kuwapa mkate na kuwaomba. Waliruhusiwa lakini wakapeleka kwenye wodi ya wagonjwa wa akili. Mgonjwa mmoja alikuwa mtu ambaye hakuongea kwa miaka mingi badala ya kutembea alitambaa. Uso wote umevimba. Sikio moja limevimba pia. Alikuwa mchafu. Wageni walimwekea mikono na kumwomba. Waliporudi wiki iliyofuata walikutana na mtu mrefu kwenye wodi hiyo. Walimomba awapeleke kwa wagonjwa. Mtu huyu alikuwa yule waliyemwomba wiki ile nyingine —maombi yao yalimbadilisha kabisa kwa hiyo alitaka kuomba tena. Hata hivyo hawakumtambua kwa hiyo waliomba tena awapeleke kwa wagonjwa. Aliwapeleka na wafanyakazi walithibitisha kwamba ni yule yule waliyemwomba wiki ile iliyopita. Wakashangaa. Huyu mtu alikuwa amepona. Alitembea na kuongea. Aliweza kuandika pia. Alianza kuonekana anaweza kupona kabisa.

Timu imeendelea kuja ikileta mkate na nguo wakaendelea kuwaomba wagonjwa. Wagonjwa wengine wakaanza kubadilika pia. Baadaye timu ikaalikwa kuwahudumia wagonjwa wote 800 pamoja na wafanya kazi wa hospitalini. Mungu aliwaongezea rasilimali ndani ya miaka mitatu timu kubwa zaidi kwa kibali cha serikali ikawahudumia watu 2600 kila wiki waliokuwemo kwenye hospitali 5, nyumba ya watoto yatima 5, jela mbili na kituo kimoja cha watu walioathirika na madawa ya kulevya. Pia walianza kuwahudumia watoto wa mtaani na watu wasio na makazi.

- Nini imetokea?
- Hayo yaliyotokea yameanzaje?
- Alifanyaje?
- Matokeo yake yalikuwaje?

- Jamii yake inafanana zaidi na mapenzi ya Mungu kutokana na vitendo vyake au la?
- Tunajifunza nini kutokana na simulizi hiyo?

Badala ya mateso uongozi

Kulikuwa na mchungaji mwingine aliyekuwa anaitwa polisi kila mara. Angalau mara sita kwa mwaka polisi ilimfuata pale alipofundisha na kumpeleka kituoni. Siku moja alijifunza dhana ya ufalme wa Mungu na akaanza kulifundisha kanisa lake. Aliwatia moyo watu wake waanze kuwahudumia jirani zao na kutafuta namna ya kuifanya jamii yao ifanane na mapenzi ya Mungu.

Makanisa yameanzisha miradi mingi: kutoa misaada, kuwajengea nyumba wajane kutengeneza barabara kujenga vyoo nk. Kanisa limekua na waumini walikomaa zaidi. Matatizo kama kucheza kamari na ulevi umeisha kwenye jamii. Watu wa serikalini wameanza kuona matunda ya kazi za mchungaji. Wakamteua kuwa kiongozi kwenye eneo hilo. Alianza kazi yake kwa kuwafundisha wafanyakazi wake somo la afya ili waende kufundisha kwenye jamii zao. Sasa afya kwenye jamii inazidi kuboreka.

- Mchungaji alifanyaje?
- Alijengaje ufalme wa Mungu?
- Matokeo yake yalikuwaje?
- Tunaweza kujifunza nini kwa ajili ya maisha yetu?

Watoto huenda shule

Kwenye eneo fulani watoto wachache tu huenda shule. Mtu mmoja akijua umuhimu wa elimu ameamua kuchukua hatua. Aliongea na watu kanisani akaunda timu ya watu waliotaka kutatua tatizo. Walienda nyumba hadi nyumba kuwatia moyo wazazi kuwapeleka watoto wao shule. Matokeo yake watu wote wakaendelea kwenda shuleni. Viongozi wakamwomba atembelee pia maeneo mengine. Matokeo yake sasa watoto wa kijijini kwake na wale kutoka vijiji vya jirani wote huendelea kwenda shuleni.

- Mtu huyu anajengaje ufalme wa Mungu?
- Ungeweza kufanya kitu kama hicho kwenye jamii yetu?

Sisi sote tunaweza kuwa watu wanaoleta mabadiliko kwenye jamii. Hawa watu hawakuwa wa pekee. Walikuwa watu wa kawaida kama sisi. Wengine walikuwa hawana elimu lakini wote walikuwa tayari kufanya wanachokiweza kujenga ufalme wa Mungu kwenye jamii yao.

Namna ya kuwa mjenzi wa ufalme

Mungu aweza kufanya anavyotaka. Angeweza kujenga ufalme wake bila kutushirikisha. Lakini kufanya hivyo si mpango wake. Mpango wake ni kututumia kwenye ujenzi wa ufalme wake. Ujenzi wa ufalme wa Mungu unaanza kwetu. Uwasomee au uwape wanafunzi kilichoandaliwa 5.2. Uwaambie waombee majibu yao.

Ugawe kilichoandaliwa 5.2–Namna ya kuwa mjenzi wa ufalme.

1. ANZA NA WEWE MWENYEWE

Hatua ya kwanza kuona ufalme wa Mungu unajengeka kwenye maisha yako, familia yako kanisa lako jamii yako na dunia ni kujitasmini. Uko tayari kutumiwa na Mungu? Uko tayari kumtii Mungu katika kila eneo la maisha yako? Wiki hii ungeweza kuboresha nini?

2. Ufundishe na kuwatia moyo familia yako

Wakati unapojenga ufalme wa Mungu kwenye kila eneo la maisha yako inabidi uitie moyo familia yako kufanya vivyo hivyo. Tunasoma tuzifundishe familia zetu muda wote. (Kumbu.6:7) bila kujali tunachokifanya. Jitahidi kufundisha familia yako kupitia matendo yako, kupitia maongezi yako, kwa kutafuta njia kuwasaidia wawasaidie wengine pia.

Kumbuka ulichoamua kufanya kwenye kipindi kwenye kila eneo kati ya maeneo manne ili familia yako ikue.

3. Mwombe Mungu akutumie kuwabadilisha wengine

Anza kuomba na kumwomba Mungu kukusaidia kuwabadilisha wengine. Tafuta fursa, unapowaona watu wenye mahitaji umwombe Mungu akuoneshe namna ya kuwasaidia watu hao. Mungu yuko tayari kutusaidia kujenga ufalme wake. Atatuonesha kwa wakati muafaka wa njia sahihi ya kusaidia.

4. Uwasaidie wengine

Ujiingize kwenye tendo la upendo na utafute namna nyingine ya kusaidia. Ikiwa unajisikia huwezi kufanya mambo mengi bado utumie vipaji vyote ulivyovipewa na Mungu kuwahudumia wengine Unapohudumia utakua na utajikuta unaweza kufanya zaidi na zaidi.

Somo la 6: Kazi ya kanisa kwenye ujenzi wa ufalme wa Mungu

Malengo makuu

1. Kuelewa kwamba kanisa lazima lihusike kubadilisha jamii ifanane na ufalme wa Mungu.
2. Kuelewa kwamba kila mmoja ndani ya kanisa ni muhimu na wote wahusike kujenga ufalme wa Mungu kwa namna moja au nyingine.

Vifaa

1. Somo la 6: Kazi ya kanisa kwenye ujenzi wa ufalme wa Mungu
2. Somo la 6: Picha zenye sehemu za mwili

Utangulizi

Kwenye somo lililotangulia tuliangalia mchakato wa mabadiliko - unavyoanzia kwako hadi familia, jamii na taifa. Hata hivyo kuna sehemu nyingine muhimu kwenye mchakato: kanisa.

Mpango wa Mungu ni kanisa lishiriki mabadiliko ili maono yatimie.

Soma Waefeso 1:22-23

- Kazi ya kanisa ni nini?
 - kukamilisha kazi ya Yesu

Soma Waefeso 3:10

- Mungu anatumia nini kuonesha hekima yake?
 - kanisa


Mistari mara nyingine si rahisi kuelewa lakini yatukumbusha kwamba Mungu amelipangia kanisa kazi maalum kwenye ujenzi wa ufalme wake. Kanisa ni mwili wa Kristo. Kazi ya kanisa ni kutimiza kazi ya Yesu kupatanisha vitu vyote.

- Kanisa lako lingefungwa lingetokea nini? Wasio Wakristo wangelalamika? Kwa nini walalamike/wasilalamike?

Lazima kanisa lisaidie jamii kiasi cha watu kulalamika wakisikia kanisa linafungwa.

Tuchore mchoro wetu kutoka kipindi kilichopita kwa namna tofauti. Tuanze na mtu, halafu familia, halafu jamii halafu taifa (Chora ubaoni.)

Kazi ya kanisa ni kusaidia mchakato. (Chora kanisa) Tuwafundishe watu, tuwasaidie kusaidia familia jamii. n.k. Pia tusaidie familia na jamii ziwe kama Mungu anavyozitaka.



Kuwawezesha watu

Maelekezo: Uwape wanadarasa picha za sehemu za mwili (Picha X).

- Zipi hazina kazi?
- Sehemu zipi ni ndogo kuliko zote?
- Hizo ndogo ndogo zisingekuwepo ingekuwaje?
- Sehemu zote zingetawanika mwili bado ungefanya kazi?
- Toa mifano kuonesha jinsi sehemu moja huhitaji zingine.
- Ikiwa sehemu zingine zisingekuwepo mwili ungewezaje

kufanya kazi? Uwaambie baadhi ya watu washushe kadi zao.

- Mwili ungeboreka?
- Kupoteza sehemu hizo ingelela shida zipi?

Waambie wanadarasa wachague sehemu zenye umuhimu zaidi halafu mfunike kadi zingine.

- Mwili ungeweza kufanya kazi sasa? Kwa nini usingeweza kufanya kazi wakati sehemu zote muhimu zipo?

1 Wakorinto 12:12-20

- Kwenye mwili kila sehemu ina umuhimu wake. Kanisa liwe kama mwili. Kila mtu kanisani yu muhimu kwenye ujenzi wa ufalme wa Mungu. Hakuna watu kanisani wasio na umuhimu. Kila sehemu ya mwili hufanya kazi za muhimu? Kuna watu wowote ambao wangeacha kuja kutokuwepo kwao kusingeathiri kanisa wala kazi zake?
- Asilimia ipi ya kanisa hushiriki? Asilimia ipi hawashiriki?
- Uwaambie asilimia hiyo hiyo ya wanafunzi kufunika kadi zao.
- Mwili wako ungekuwa na asili mia ndogo kama hiyo ya sehemu zinazofanya kazi mwili wako ungekuwaje? Hayo ni kweli pia kwa kanisa? Kanisa lingefanya vizuri zaidi kama watu wengi zaidi wangeshiriki?
- Tufanyaje kukabiliana na shida hiyo?

Kwa nini lazima wote tutoe huduma?

Soma Waefeso 2:10

- Tuliokolewa ili tufanyeje?
- Watu wote waliokolewa wafanye matendo mema au baadhi yao tu?
- Watu wote kanisani kwako hutenda matendo

mema? Soma simulizi ya talanta (Mathayo 25:14-30)

- Unaposoma simulizi hiyo unafikiri inaonesha kwamba si kila mtu anapaswa kutumia talanta zake kuujenga ufalme wa Mungu?
- Wakristo wote hutumia talanta zao kikamilifu?
- Tufanyaje ili watu wengi zaidi watumie talanta zao kikamilifu kujenga ufalme wa Mungu?

Lazima tushirikiane WOTE ili tujenge ufalme wa Mungu. Wakati mtu mmoja anaweza kujenga sehemu ndogo ya ufalme wa Mungu tutaweza kujenga ufalme wa Mungu vizuri zaidi pale ambapo kanisa zima hujenga ufalme wa Mungu kwenye maeneo yote ya maisha yao halafu linawasaidia wengine kufanya vilevile. Fikiria kila mtu kanisani angejitahidi kutekeleza mapenzi ya Mungu kwenye maisha yake binafsi kanisani au kwenye jamii. Wangefanya hivyo ingeleta mabadiliko gani kwenye jamii?

Waefeso 4:11-12

- Viongozi wana nafasi gani? (mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na walimu)?
- Kwenye makanisa mengi wanasema 10% ya watu hufanya 90% za kazi. Ni kweli? Tutawezaje kuibadilisha hali hii?
- Tuwajengaje wengine ili waweze kutoa huduma na wao?

Mara nyingi husemwa wanaotoa huduma hujifunza zaidi. Indonesia kulikuwa na wamishonari waliofanya kazi na vijana. Pamoja na kuwafundisha kila wiki walianza kuchoshwa na udhaifu wa Wakristo na kwa sababu ya ukuaji wao. Waliamua lazima vijana waanze kutoa huduma Kwa hiyo waliunda sheria mpya kusema kwamba wale tu ambao hutoa huduma huruhusiwa kushiriki kwenye mafunzo ya kila wiki. Vijana wengi zaidi wameanza kushiriki mambo mbali mbali. Waliwasaidia familia masikini kwenye jamii, wakawafundisha watoto na wakatoa huduma za kiroho kwa watoto. Baada ya miezi michache vijana walikuwa wameshakuakiroho. Sasa ikawabidi wasome biblia na kuomba. Wakamtumainia Mungu awasaidie kuwasaidia wengine.

Majadiliano kwenye kundi kubwa

- Nini kimetokea kwenye simulizi hiyo?
- Vijana walitumia njia zipi kuhudumia?
- Umeshawaona watu wakikua wanapojihusisha kutoa huduma kanisani ?
- Kwa nini watu hukua wanapotoa huduma?

Kubadilisha Familia

Kanisa laweza kuwasaidia familia kuishi kufuatana na mapenzi ya Mungu likiwafundisha wanakanisa jinsi ya kuwa na ndoa thabiti, kuwa wazazi bora na kuwapa familia nafasi kuabudu na kutoa huduma pamoja. Lazima kanisa litafute fursa kusaidia watu kuzihudumia familia zao na kusaidia familia kuishi kufuatana na mapenzi ya Mungu.

Kubadilisha jamii

Kama kanisa twaweza kubadilisha jamii kwa namna tofauti tofauti. Njia tatu muhimu ni:

1. Kuongeza idadi ya Wakristo

Hiyo haimaanishi kuongeza idadi ya watu kanisani (twaweza kuongeza idadi kwa kuiba kondoo kutoka makanisa mengine) Kuongeza idadi ya Wakristo humaanisha kwamba wasio wakristo wanamjua Mungu na wanamkubali Kristo kama mwokozi wa maisha yao. Makanisa huwasaidia watu kuelewa injili na kuwalea Wakristo wapya.

2. Kufundisha jamii kuishi kwa kumtii Mungu

Kama tulivyojifunza Mungu ametuumba na anajua mahitaji yetu. Alituonesha namna ya kuishi kwenye Biblia. Tunaweza kuwafundisha wengine kanuni za msingi za Biblia. Kama kanisa mnaweza kutafuta njia kuwasaidia watu watii kwenye kila eneo la maisha yao. ,

Hata wale wasiotaka kupata habari ya Ukristo labda watapenda kupata habari za afya, ndoa thabiti au namna ya kutunza fedha kwa hekima. Mafunzo hayo huwasaidia watu kujenga maisha yao wakiishi kutokana na kanuni za kikristo na pia husaidia kujenga mahusiano mema kati ya wasio wakristo na kanisa.

3. Uzisaidie jamii zao kuishi kutokana na mapenzi ya Mungu kupitia miradi ya huduma

KWENYE VIKUNDI VIDOGO

Jibu maswali yafuatayo:

- Mathayo 20:28—Yesu amekuja kwa sababu gani?
- Phil 2:4-9—Paulo anamwelezaje Yesu?
- Yesu amekuja kutoa huduma. Biblia inaposema “kuwa Mungu kiasili” inaweza kusomeka pia **“kwa sababu alikuwa Mungu”**, Hakuona ni muhimu kuwa sawa na Mungu badala yake amejishusha akiwa mtumishi halisi. Fikiria kwa sababu yeye ni Mungu amejishusha kabisa akiwa mtumishi halisi. Asilia ya Mungu ni kutoa huduma. Kwa sababu kanisa ni mwili wa Kristo asili ya kanisa pia iwe kutoa huduma.
- Yakobo 1:27—Mungu anataka dini ya aina gani?
- Marko 12:31—Mungu anatumrisha tufanyaje?

Upendo wetu kwa Mungu na kwa wengine utufanye tutoe huduma. Jinsi Kristo alivyokuja kuhudumia madhumuni ya kanisa ni kutoa huduma kwa kuwasaidia watu wamjue na kukua ndani ya Yesu na kwa kuonesha upendo wake kwao.

Tunapozihudumia jamii zetu zitabadilishwa. Soma simulizi ya jamii iliyobadilishwa kutokana na huduma za kanisa.

Shule ya Jamii

Kagishu, eneo la pembeni la mji lenye nyumba za mabati na mbao lilikuwa na kanisa lenye waumini 15. Kanisa limealikwa kwenye mafunzo ya HUDUMA KAMILIFU wakamchagua Meshack mwenye miaka 21 ahudhurie. Meshackamerudi na maono: “Nimejifunza kumtii Yesu si hiari!” Kwa hiyo Meshack, Dismus (Mzee wa Kanisa), mchungaji na mke wake wakaomba wakamomba Mungu mradi wa kuonesha upendo wa Mungu kwenye jamii. Wakapata jibu: anzisheni shule ya msingi kwa ajili ya watoto kanisani.

Papo hapo wakaanza kuongea na waumini walioshindwa kulipa ada ndogo za shule za kiserikali Watu kadhaa wakakubali kuleta watoto wao kwenye shule mpya. Bila mafunzo yoyote Meshak, mchungaji na mama mchungaji wakaanza kuwafundisha watoto 13 wenye umri kati ya miaka 6-12. Walikuwa na chumba kimoja kisichokuwa na madawati vitabu wala vifaa. Wanavijiji hawakutaka kushirikiana na shule bali wakaja usiku kuiba vifaa vya ujenzi. Mshahara wa kwanza wa Meshak umeingia baada ya mwezi 1 dola 1 iliyotolewa na wazazi.

Mesack na Dismus waliwaalika watoto wa majirani na shule ikakua. Watoto wakafika 45 wenye umri tofauti tofauti kwenye chumba kimoja. Baada ya miezi 6 mwalimu mwingine akajitolea na baada ya miezi minane mwalimu wa tatu akajitolea. Wakiwa na watoto 100 walimu wamesimama kati kati kila mmoja akatazamana na wanafunzi wake huku wakipeana mgongo. Majirani wakaanza kuhama na shule ikapata nafasi zaidi Shule ilipofikisha miaka miwili ilikuwa na majengo mawili yenye vyumba zaidi ya 10 ambavyo vikatumika pia kwa ajili ya kanisa kila jumapili.

Mwaka uliofuata kanisa lilionua kiwanja Kawangware likanunua jengo likahamia mle. Baada ya miaka 6 kulikuwa na walimu 17 wenye mshahara wafanyakazi wengine watano na watoto 445.

Hapo ni mwanzo tu wa historia ya jamii, shule na kanisa. Matokeo ya jitihada hizo ni kuwa na shule ya sekondari kwenye kijiji jirani. Shule hii ina wafanyakazi kumi na watoto sitini. Kanisa jingine limeanzisha mahali pa kuhifadhi watoto mama zao wanapokuwa kazini. Kanisa la awali likakua wakafikia waumini 60 likaanza kanisa jingine lenye waumini zaidi ya 40. Kila kanisa limeanzisha makanisa mawili mapya kwenye maeneo tofauti tofauti.

Miaka 6 baada ya kujitolea kwenye utiifu kwenye kanisa dogo kuna matokeo makubwa yanayoonekana wazi kwenye jamii na makanisa ya eneo hilo. Wanajamii wakathibitisha mabadiliko hayo walipopendekeza wabadilishe jina la eneo lao kutoka Kagishu (maana yake “kisu”) Kuwa Ruita (maana yake “kuondoa hatari”).

Majadiliano kwenye kundi kubwa

- Nini kilichotokea kwenye simulizi hiyo?
- Kanisa lilikuwa na watu wangapi?
- Matokeo ya matendo yao yalikuwaje?

Kwenye kijiji kimoja wanavijiji walikuwa wanasaidiana wakati wa mavuno. Hata hivyo yule aliyesaidia alipaswa kutoa chakula na vinywaji kila siku. Gharama hiyo iliwafanya wakulima wakose faida kutokana na kilimo chao.

Kanisa liliamua kwa upendo kuwasaidia familia masikini bila malipo wakileta chakula chao wenyewe. Wanajamii wengine walipoona hayo wakaanza pia kusaidiana bure bila kudai chakula na vinywaji.

Siku hizi wanasaidiana bila kupewa chakula na pombe. Wakulima walianza kupata faida na mavuno yanayowatosheleza kwa mwaka mzima.

- Kanisa limefanyaje kusaidia jamii?
- Matokeo yake yalikuwaje? Jamii imebadilikaje?

MAJADILIANO KWENYE VIKUNDI VIDOGO

- Kanisa letu linaweza kufanyaje kusaidia jamii?
- Kanisa letu linaweza kuwasaidia watu kuishi kuendana na mapenzi ?

SOMO LA 7: Programu ya mabadiliko kwa msingi wa ukweli

Lengo kuu

1. Programu ya mabadiliko kwa msingi wa ukweli yahusu kuyawezesha makanisa kubadilisha jamii

Vifaa

1. Somo la 7: Maono ya mradi
2. Somo la 7: Posta ya kanisa hubadilisha jamii
3. Somo la 7: Mada za mafunzo yajayo

Utangulizi

Watu wawili wajitolee wasimame katika pande tofauti za meza. Waambie wavute meza kwa mwelekeo tofauti kila mtu upande wake. Baada ya dakika moja au mbili, uwaambie kwa pamoja waipoleke/waibebe meza hiyo katika mwelekeo mmoja.

- namna ipi ilikuwa rahisi – wakielekea mwelekeo mmoja au wakivutana kila mmoja akitaka kwenda kwingine?

Kwenye vipindi vilivyopita tulizungumzia ufalme wa Mungu. Sisi kama shirika tunatamani kujenga ufalme wa Mungu duniani. Maono yetu kwa ajili ya mradi ni (uoneshe posta au uandike ubaoni):

kuyawezesha makanisa kuzibadilisha jamii zao

Maono yetu ni tunachotaka kuona baada ya kujiunga na ninyi. Mnaposikiliza mfikirie kama nanyi mnalipenda hilo kumbukeni mfano wa meza. Wakati gani kubeba meza kulikuwa rahisi? Mlipoelekea sehemu ile ile. Hivohivo mnaposhirikiana mkiwa na malengo tofauti hamtaelewana. Hatutashirikiana vizuri. Tunapokubaliana sisi sote kujenga ufalme wa Mungu tutaenda sambamba. Tutashirikiana vizuri.

Maono ya mradi

Kuyawezesha makanisa kuzibadilisha jamii zao

Kuwezesha makanisa

Kama tulivyosema kwenye somo lililopita kanisa ni muhimu kwenye ujenzi wa ufalme wa Mungu. Kanisa husambaza maono na hufundisha na huwasaidia watu wanaoyatekeleza. Tunatamani kusaidia makanisa kufanya kazi zao. Hatutaki kuchukua kazi zao kutoka kwao (Onesha picha 5)

Kuyawezesha makanisa **hayamaanishi:**

1. Twajua kila kitu—kila eneo liko tofauti lenye hali tofauti. Tutajifunza pamoja namna ya kuisaidia jamii yako.
2. Huna uwezo—kila moja wetu ana kipaji chake, ujuzi na uwezo wake. Mkitumia yote mlichopewa na Mungu mtaweza kubadilisha jamii yenu. Tutawaletea mawazo na ujuzi mnaouhitaji.
3. Tutatawala kinachoendelea—kanisa na jamii ni ya kwenu. Ninyi mnajua kinachohitajika kifanyike. Kama tulivyopendekeza vitendo vya upendo vivyo hivyo tutatoa mapendekezo lakini hatutawaambia mfanyaje. Mtaamua mradi gani utakaowafaa zaidi kwenye eneo lenu.
4. HILO HALIHITAJIKI KOTE WAVEZA KULIACHA) tunaanzisha dhehebu au tunataka ubadilishe dhehebu lako. Siyo hivyo tena ni kinyume chake. Usibadili dhehebu na usipingane na kiongozi wako. Angalia Daudi alivyomfanyia Saulo. Daudi alimchezea nyimbo Saulo wakati Saulo alimrushia mikuki. Alipotishiwa maisha Daudi aliondoka peke yake. Hakujaribu kuchukua nafasi ya Saulo na hakuwaomba watu wamfuate hata kama Mungu alimwahidi ufalme. Alipopata nafasi hakumwua Saulo alimwachia maisha yake.

Tunawatia moyo watu wawe kama Daudi. Hata kama una kiongozi mbaya endelea kumfuata na kumombea. Mambo yakizidi uondoke peke yako. Usiende na mtu isipokuwa mke na watoto wako. Usipambane na kiongozi wako. Kama Daudi uogope kumsema vibaya.


Kama viongozi kwenye shirika hilo tunakata tama tukiona jinsi makanisa na viongozi hubadili madhehebu Hatuamini hilo linamtukuza Mungu. Uwe kama Daudi uwe mwaminifu kwa viongozi hata kama inakuwa vigumu. Hayo yanamtukuza Mungu.

Sisi kama shirika hatupendelei dhehebu na hatuendani na dhehebu lolote. Tunashirikiana na madhehebu mengi. Wanachama wa timu yetu hutokana na madhehebu mbalimbali. Tunataka makanisa yote yaendane na mapenzi ya Mungu. Tunaamini Mungu anaweza kujenga ufalme wake kupitia madhehebu mbalimbali.

Hayo **yanamaanisha:**

1. Tutakufundisha kubadilisha jamii yako. Hatutatuma wafanyakazi wetu kwenye jamii yako kuibadilisha Tunaamini kanisa ni kifaa cha Mungu cha kuleta upatanisho tutakusaidia unapofuata mapenzi yake.
2. Ni maono yako na mapenzi yako. Tutapendekeza mawazo mengi lakini ni jukumu lako kuchagua mawazo na miradi gani utakayotekeleza kwenye kanisa lako Hulazimishwi kuchagua mojawapo ila ukiamua kuona ujenzi wa ufalme wa Mungu kwenye jamii yako tunakutia moyo utekeleze miradi mingi iwezekanavyo. Tulipoyatembelea makanisa tuliona yale yaliyotekeleza miradi mingi yaliona mabadiliko makubwa. Yenye miradi michache yaliona mabadiliko madogo.

Inategemea malengo yako Kubadilisha jamii ni kazi ngumu.



Kubadilisha jamii

Sehemu ya kwanza ya maono yetu ni kuwezesha kanisa. Sehemu inayofuata ni yale tunayoyawezesha makanisa kufanya: kubadilisha jamii.

Kubadilisha

- Kwa nini tunatumia neno la kubadilisha? Kubadilisha humaanisha nini? Kitu kinapobadilishwa kinabadilika kabisa kwa namna ambapo huwezi tena kurudisha hali yake ya awali. Kwa mfano ufikirie kiwavi na kipepeo. Kiwavi kinabadilika kuwa kipepeo. Hakiwezi kurudishwa kwenye hali yake ya awali. Mabadiliko yako kamili. Tunataka kuona mabadiliko kwenye jamii zetu. Tunataka kuona jamii zilizobadilishwa kuishi kutokana na mapenzi ya Mungu wala hayarudi kwenye hali zao za awali baada ya miaka kadhaa.

Maeneo ya mabadiliko

Vikundi vidogo

Uliza kila kikundi wataje mabadiliko wanayoyataka kwenye jamii zao chini ya vichwa hivyo — kiroho kijamii kiakili na kimwili— yakiwa kama matokeo ya programu. Uwakumbushe kwamba kijamii huhusiana na mahusiano kwa mfano: ndoa, kuwa wazazi, mahusiano kati ya majirani nk. Kimwili ni pamoja na pesa, kazi, afya nk Wanaweza kutumia mawazo waliyoyapata kwenye somo la kwanza.

Wakimaliza washirikishe wenzao. Kuna kitu ambacho vikundi karibu vyote au vyote vimeandika? Kitu gani?

Andika chati ifuatayo ubaoni. Uwaambie waangalie mada chini ya vichwa vya kijamii, kiakili kimwili na kiroho. Upitie kila eneo kwa kujadili maswali hayo mawili kwa kila maada

kiroho	kimwili	kijamii	kiakili
idadi ya juu- uinjilisti	<ul style="list-style-type: none"> mapato zaidi kilimo matumizi bora ya pesa 	kusaidiana	elimu
kukua kiroho—kuwa wafuasi	nyumba bora	ndoa bora	kusoma kuandika
	afya bora	kuwa wazazi bora	

Majadiliano ya kundi kubwa

- Kuna tofauti gani kati ya malengo yenu na ya kwetu?
- Kati ya malengo yetu kuna mengine unayoyashangaa au usiyokubaliana nayo?

Ukiyaangalia maeneo yote ma tatu jadili:

- Unapoangalia orodha za malengo unafikiri zinafanana vya kutosha ili tuweze kushirikiana?

Mbinu

Hii ni programu ya mafunzo Hatutoi pesa kuendesha programu. Kama tutakavyojifunza huko mbeleni si kwamba sisi ni masikini kwa sababu hatuna rasilimali. Na hatutaondokana na umasikini kwa sababu tutapata rasilimali. Peter anasema kwenye matendo ya mitume:3:6, “Sina fedha wala dhahabu lakini nitakupa nilicho nacho” Upande wetu sisi tuna ujuzi na mawazo yatakayoiwezesha jamii yako kufanana na mapenzi ya Mungu. Tunaamini mafunzo hayo na kujitolea kwako na jitihada zako na uwezo wa Mungu wa kuzidisha kutabadilisha taifa letu.

Tunatoa mafunzo kwa mtu yeyote kanisani kukusaidia kuwa na mawazo na uwezo unaohitaji kukusaidia kubadilisha jamii yako

Mada za mafunzo yajayo.

Onesha picha 7 inayoeleza mada zijazo. Eleza tumepanga kufundisha hayo ila mabadiliko yaweza kutokea .

Somo la 3 – Uwongo wa Shetani unavyotuathiri na jinsi ya kupingana nao

Somo la 4 – afya

Somo la 5 – ndoa

Somo la 6 – utunzaji fedha

Somo la 7 – chumvi na taa

Somo la 8 – kilimo

Somo la 9 – kutangaza neno la Mungu

Somo la 10 – Kuishi anavyotaka Mungu

Mada nyingine —kwa mfano afya ndoa familia kilimo na utunzaji fedha — ni pamoja na mafunzo ya vikundi vidogo. Yaweza kufanyika na kanisa na jamii. Unapopitia mafunzo hayo tutakufundisha jinsi ya kutumia mawazo hayo kwenye kanisa lako na jamii yako. Tutakupa mambo ya kutekeleza.

Somo la 8: Hatua zifuatazo

Lengo kuu

1. Lazima tupange na tufanye kazi kwa malengo.

Vifaa

1. Kilichoandaliwa 8.1 Vitendo vya upendo hatua za kupanga

Umuhimu wa kupanga

Mr. Lim, mkulima, ameenda kuanda shamba lake kwa kilimo. Njiani alikumbuka kwamba mke wake alimwomba kulisha kuku akarudi nyumbani akachukua chakula cha kuku akawapa. Alipokuwa anawalisha kuku akaona zizi la mbuzi liliharibika. Aliogopa mbuzi watakimbia akarudi nyumbani kutafuta nyaya kutengeneza zizi. Alipokosa vifaa akaenda kwa jirani yake Mr. Son akaomba vifaa. Kwa jinsi ameshafika huko akaamua kutumia muda kidogo kuongea na Mr. Son, mkristo mpya aliyekuwa na shida kidogo.

Ilipofika 5:30 mke wa Mr. Son akamkaribisha chakula cha mchana. Alipoona muda akaomba msamaha na kurudi nyumbani ale na familia yake. Baada ya kulala kidogo ameenda kutengeneza zizi. Akiwa kazini mke wake alimkumbusha kwamba pampu kwenye kisima ilikuwa imeharibika. Kwa jinsi alikuwa na vifaa akaamua atengeneze. Ilipofika jioni alikaribia kumaliza kutengeneza pampu. Hata hivyo alikuwa hajaenda kulima lakini amerizika akijua kesho yake angemaliza kutengeneza pampu na kurudisha vifaa halafu ataenda kulima.

- Nini kilichotokea?
- Vitu alivyovifanya vilikuwa vya ovyo au vya lazima?
- Nini kitatokea akiendelea namna hii bila kupata nafasi ya kulima?
- Tutaonyaje tusiwe kama mkulima huyu?

Miradi mingi huendeshwa kama siku ya mkulima huyu. Tunashughulika mno kufanya vitu vizuri kimoja baada ya kingine hadi vitu muhimu havifanyiki kwa sababu tunashughulika na vitu vya haraka. Matokeo yake hatufanyi vitu muhimu. Mbaya zaidi mara nyingine maisha yetu ni kama maisha ya mkulima. Tunakimbia hapa na pale bila kufikiria kipi ni muhimu ili tukifanye Kitu cha kwanza kabisa tuamue nini ni muhimu zaidi. Tukijua kilicho muhimu tutaamua vizuri jinsi ya kutumia muda wetu. Vitu gani unapaswa kufanya ndani ya miezi mitatu ijayo ili ufaulu?

- Kuwafundisha wengine— tukitaka sehemu nyingi zaidi za mwili zitoe huduma lazima tufundishe masomo tuliyoayasoma.
- Kuratibu vitendo vya upendo—lazima tuendeleze vitendo vya upendo mara kwa mara.
- Kukutana mara kwa mara

Mikutano

Uchague kikundi mkutane mara kwa mara kupanga vitendo vya upendo. Mara nyingi ni kamati kanisani na mnakifanya wakati wa kamati kukutana mara kadhaa kila mwezi

- Mnapokutana mfanyaje?
 - Kuomba—ni kwa nguvu za Mungu tunapoweza kubadilisha jamii zetu. Tukitaka mabadiliko lazima tuombe pamoja.
 - Kuamua vitendo vya upendo vipya
 - Mtafute mawazo namna ya kusaidia jamii zako

Wakati wa mikutano yenu mchukue muda wa kuomba na kujadili mahitaji ya jamii. Mwombe kama mnatakiwa kusaidia na kwa jinsi gani msaidie. Mjadili kitendo cha upendo kiilichopita kujua kipi kimeenda vizuri na wapi kulikuwa na shida. Mjiulize mnapaswa kubadili nini safari ijayo?

Vitendo vya upendo

Angalia picha ya jamii uliyoichora kwenye somo la 1.

Angalia picha zote mtengeneze orodha ya mabadiliko yanayotakiwa ili picha ziwe kweli. Kwenye kikundi mwombe jinsi ya kuleta mabadiliko. Chagueni badiliko mmoja na pamoja mpange kitendo cha upendo kuleta badiliko hilo

Pitia fomu ya kitendo cha upendo (ukurasa unaofuata) na utengeneze mpango.

Vitendo vya upendo Hatua za kupanga

Hatua ya 1: Maombi

Kwanza ni kuomba. Uchukue nafasi sasa kuomba. Mwambie Mungu akuoneshe ufanye nini kama kitendo chako cha upendo.

Hatua ya 2: Kuchagua kitendo

Kama kikundi mwamue mnaweza kufanyaje kuonesha upendo wa Mungu. Tazama baadhi ya mawazo uliyoyataja kwenye kipindi 1 halafu mkubaliane Mungu anawaongoza kufanyaje.

Mkishachagua jambo hakikisheni mnaweza kukifanya ndani ya siku moja au mbili. Ikiwa haiwezekani mnaweza kukifanya ndani ya hatua moja au mbili?

Hatua ya 3: Amua kuhusu mahitaji

Hatua inayofuata ni kuanza kupanga. Kwanza tuamue kuna mahitaji yapi – watu gani wanahitajika, vifaa vipi, ruhusa zipi nk. Kukusaidia utumie karatasi ya kazi kwenye daftari lako la mwanafunzi. Ukishajaza safu ya kwanza na mahitaji unaamua nani atakayehusika na kazi iwe imekamilika lini.

Hatua ya 4: Andika mpango

Ukishapanga mambo yote uandike mpangilio kutokana na tarehe ili ujue nani anapaswa kufanya nini wakati gani. Uchague kiongozi wa mradi. Kazi yake ni kuwasiliana na wahusika siku moja kabla ya tarehe husika kujua kama wameshamaliza, kama kuna matatizo na ikiwa wanahitaji msaada.

Hatua ya 5: Omba

Baada ya kumaliza kuandika mpango uombe tena. Mwombe Mungu akusaidie kukamilisha kitendo. na kuzidisha matokeo ili jina lake litukuzwe. Kwa wiki mbili zijazo unapoandaa kitendo chako cha upendo umwombe Mungu akusaidie na kitendo chako.

Hatua ya 6: Tenda kitendo cha upendo

Hatua inayofuata ni kutekeleza kitendo cha upendo ulichokipanga. Anza siku kwa maombi na umkabidhi Mungu jitihada zako. Kumbuka unafanya hivyo kuonesha upendo wa Mungu kwa jamii yako. Uwe na mtazamo unaoendana na lengo hilo.

Hatua ya 7: Tasmini na utoe taarifa

Hatua ya mwisho ni kutoa taarifa na kutasmini. Kwa nini tunatasmini? Kwa sababu inatusaidia kujifunza. Tunafikiria kilichoenda vizuri na wapi tunahitaji kuboresha safari ijayo. Si lazima kutumia muda mrefu utumie muda mfupi tu kujadili maswali yafuatayo:

- Nini kimeenda vizuri?
- Kitu gani hakijaenda vizuri?
- Safari ijayo unaweza kuboresha nini?
- Matokeo yalikuwa kama ulivyotegemea ikiwa hamna kwa nini?
- Mungu alitukuzwa?

Mwendeshaji ana fomu ya kutoa taarifa. Kwa nini tunatoa taarifa? Kwenye Marko 6:30 tunaona kwamba wanafunzi walitoa taarifa ya mambo yote waliyoyafanya . Tunatoa taarifa kama shukrani kwa waliotufundisha na kutuandalia vifaa. Kutoa taarifa kunakupa nafasi kueleza ulichokifanya na kutoa ushuhuda jinsi Mungu alivyotumia jitihada zako. Pia inawasaidia waendeshaji kugundua matatizo na kukuhudumia vizuri zaidi huko mbeleni.